

ELIMU

‘Wengi wanaugua ‘ukichaa’ bila kujijua’

Elias Msuya, Mwananchi
emsuya@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Mwenyekiti wa Chama cha Watoa huduma ya afya ya akili Tanzania (Mehata), Dk Isaac Lema, amesema idadi kubwa ya watu wanaugua magonjwa ya akili mpaka kufikia kuwa vichaa bila kujijua kwa sababu ni tatizo lisilopewa kipaumbele.

Lema alitoa kauli hiyo juzi katika uzinduzi wa tovuti ya taasisi ya Tap Elderly Women’s Wisdom for Youth (TEWWY) uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Taasisi hiyo ya wanawake wazee imejikita kutoa ushauri kwa watu wenye magonjwa ya akili na kuwafikisha kwenye vituo vya kutolea huduma kwa ajili ya matibabu.

Lema alisema pamoja na kwamba hakuna takwimu za jumla kitaifa, lakini kumekuwa na ongezeko la wagonjwa wa akili wengi wakiwa wanaume.

“Utafiti uliofanyika kwa mkoa wa Dar es Salaam miaka ya 2000, uligundua kuwa kati ya watu 100 watu wanne mpaka watano walishapata ugonjwa wa akili na magonjwa yenyewe ya akili ni yale yaliyofikia katika hatua kubwa.

“Hospitali ya Taifa ya Muhimbili walitoa takwimu kwamba kulikuwa na ongezeko la wagonjwa takribani zaidi ya 22,000 waliofika kuhudumiwa na ongezeko ni kwa

NUKUU

“Mambo yamebadilika sana, mtu kuokota makopo siku hizi ni kwa ajili ya biashara, nguo kuchanika ni mtindo, kutochana nywele pia ni mtindo, kwa hiyo huwezi tena kutumia kama kiashiria,”

Mwenyekiti wa Chama cha Watoa huduma ya afya ya akili Tanzania (Mehata), Dk Isaac Lema.

wanaume na moja ya kisababishi ni matumizi ya vilevi,” alisema Dk Lema.

Hata hivyo, alisema licha ya kuongezeka kwa wagonjwa wa akili, bado kuna changamoto ya uelewa wa jamii kuhusu magonjwa hayo. “Wengi wanaelewa tatizo moja la akili, lakini magonjwa ya akili yapo zaidi ya 100. Wengi ukiwaambia mtu anapitia dalili za ugonjwa wa akili, wanauliza mbona hajachanganyikiwa? Mwingine anauliza mbona naongea vizuri?”

Alisema kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha, watu wanashindwa kuelewa viashiria vya ugonjwa wa akili kwa kuwa siku hizi kumekuwa na mabadiliko ya tabia zilizodhaniwa kuwa ni dalili ya ukichaa.

Alisema miongoni mwa magonjwa ya akili yanayowatesa watu

ni kushuka kwa hisia kunakosababishwa na matukio hasi kama kufukuzwa kazi, kufeli masomo au kufiwa.

“Mtu anakuwa kwenye huzuni zaidi ya wiki mbili na kunakuwa na mawazo hasi ya kumwonyesha kuwa yeye hana maana, maisha hayana maana hatimaye wengine wanapata mawazo ya kujidhuru na pia inakuja na hali ya kutojumuika na watu wengine,” alibainisha.

Alisema kutokana na ukubwa wa ugonjwa huo, Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (WHO) linakadiria kuwa ifikapo mwaka 2030 utakuwa ni miongoni mwa magonjwa yanayosababisha mzigo katika jamii duniani kuliko hata kisukari.

Carolyne Swai ambaye ni mmoja wa wanachama wa TEWWY alisema wamepata mafunzo ya kubaini dalili za watu wenye ugonjwa wa akili na kuwapeleka kwenye vituo vya afya kupata matibabu.

“Tunakwenda kwenye ushauri, tunauliza maswali na kusikiliza maelezo ndipo unajua tatizo la mtu na ndio unamsaidia kwa kumpa ushauri,” alisema Swai.

Mkurugenzi wa taasisi ya TEWWY, Rustika Tembele, alisema tovuti hiyo itarahisisha upatikanaji wa taarifa za magonjwa ya akili na kutoa msaada ili kukabili-ana na magonjwa hayo.

Uhaba wa mikopo watesa wanawake

“Changamoto tunayokabili-ana nayo ni kukosa mitaji. Tunajua kuna mikopo inayotolewa na halmashauri, lakini foleni ni kubwa inachukua muda mrefu kupata,”

Mjasiriamali
Beatrice Ndossi

Elias Msuya, Mwananchi
emsuya@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Licha ya juhudi zinazofanywa na wanawake wajasiriamali nchini, changamoto za mitaji na ukosefu wa uhakika wa biashara zao ndiyo kimekuwa kikwazo kikubwa kwao.

Kikwazo hicho kimetajwa na Beatrice Ndossi, ambaye ni mjasiriamali aliyeamua kuunganisha wanawake wenzake kuunda vikundi vya kujiinua kiuchumi.

“Tulianza mwaka 2019 na mpaka sasa nimeshaanzisha vikundi vinne ambavyo ni Mkombozi, Amani, Ebenezer vyote vya Dar es Salaam na kingine nimekianzisha Bagamoyo mkoani Pwani, bado hakijapewa jina,” alisema Ndossi.

Hata hivyo, alisema wamekuwa wakichangishana katika vikundi vyao na kufanya biashara zao. Pia alisema wamejiunganisha na taasisi nyingine zinazotoa mikopo kwa wajasiriamali na baadhi wamepe-ewa mikopo.

Naye mwanakikundi cha Mkombozi yupo, Lucy Kway, mkazi wa Tabata jijini Dar es Salaam, alisema ugonjwa wa corona umevuruga mipango yao na wameshindwa kufikia malengo.

“Tulianzisha kikundi cha Mkombozi mwaka 2019 tukilenga kujitendeza kibiashara na kusaidia kijamii. Kila mwanachama alitakiwa kutoa ada ya Sh27,000 kwa mwezi, lakini janga la corona, wanachama hawakuweza tena kutoa michango,” alisema Kway.

Alisema awali walikuwa wanachama wapatao 20, lakini walikuja kupungua karibu nusu kwa sababu baadhi yao hawakutoa michango.

Wakwama kupata dhamana Kisutu

Hadija Jumanne, Mwananchi
hjumanne@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Meneja wa Kampuni ya M/S Badr East African Enterprises Limited, Badr Mohamed (59) na wenzake wawili wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kujibu mashitaka 13, yakiwamo ya kuongoza genge la uhalifu, kughushi na kujipatia zaidi ya Dola 10,710,892.51 kwa njia ya udanganyifu.

Mbali na Mohamed, washitakiwa wengine katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi ni Ahmed Al-Katiy (69) ambaye ni Mkurugenzi na Mhasibu wa kampuni hiyo, Akil Hassanali (56). Washitakiwa hao walifikishwa mahakamani hapo jana na kusomewa mashitaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Augustina Mbanda.

Hata hivyo, kabla ya kusomewa mashitaka hayo, Hakimu Mbanda aliwaeleza washitakiwa hao kuwa wanashitakiwa na kesi ya Uhujumu Uchumi kwa hiyo hawatatakiwa kujibu chochote.

Akiwasomea mashitaka hayo, Wakili wa Serikali Estar Martin, akisaidiana na Yusuph Aboud, alidai kati ya Oktoba 24, 2016 hadi Agosti 31, 2018 washitakiwa hao waliongoza genge la uhalifu kwa kufanya udanganyifu na kujipatia Dola za Kimarekani 10,661,074.69 mali ya Serikali ya Tanzania

Katika shtaka la pili, washitakiwa wanadaiwa kabla ya Oktoba 24, 2016 eneo la Tabata Matumbi Wilaya ya Ilala, walighushi nyaraka ya malipo ya awali namba CRD 16-IGT 815 ya Oktoba 24, 2016 wakionesha kwamba ime- tolewa na Benki ya CRDB kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa ajili ya kutoa malipo ya awali kwa Kampuni hiyo kiasi cha Dola za Marekani 5,287,363.91 wakati akijua si kweli.

MSAADA

Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard (katikati) akimkabidhi msaada wa bati na vifaa vya ujenzi Waziri wa Kilimo Maliasili na Umwagiliaji Zanzibar, Soud Nahoda Hassan wakati wa makabidhiano ya vifaa vya ujenzi yakiwemo mabati 200 kutoka benki ya NMB kwa ajili ya shule ya Sekondari Jambiani. Picha na mpiga picha maalum.

